JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

12 JULAI, 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 12 JULAI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2010/2011.

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2008/2009 *[The Annual Report of Tanzania Education Authority for the Year 2008/2009].*

MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na

Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2008/2009 *[The Annual Report and Audited Accounts of The Local Authorities Pensions Fund* **(LAPF)** *for the Year 2008/2009].*

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

201. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mojawapo ya vyanzo vya migogoro katika Shule za Sekondari za Kata katika Jimbo la Mwibara ni Bodi za shule hizo:-

(a) Je, Serikali inatambua hilo;

(b) Je, ni sifa/vigezo gani vinatumika kuwachagua Wajumbe wa Bodi hizo;

(c) Je, Serikali imefanya juhudi gani za kumaliza tatizo hilo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

202. MHESHIMIWA ABDUL JABIR MAROMBWA (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kituo cha Polisi cha Kibiti ni Kituo pekee katika Jimbo la Kibiti lakini kimejengwa katika hifadhi ya barabara (*road reserve*) ya Kibiti – Lindi na kimechakaa sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukihamisha Kituo hicho na kukijenga katika kiwanja kipya Kibiti;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia askari wa Kituo hicho vifaa vya kufanyia kazi ikiwemo gari na pikipiki.

(c) Je, Kituo hicho kitarajie kupata kitu gani katika Mwaka huu wa Fedha 2010/2011.

WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

203. MHESHIMIWA CYNTHIA HILDA NGOYE (VITI MAALUMU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Mawasiliano ya simu za mikononi katika vijjiji vya kandokando ya Ziwa Nyasa, vya Mikoa ya Mbeya na Iringa hayajawahi kuwepo tangu huduma hiyo ianzishwe nchini:-

Je, ni lini Serikali itazihimiza Kampuni za simu za mikononi kuwekeza katika vijiji vya Ikombe (Kyela), Lumbila, Nsele, Makonde, Lifuma, Nsisi na Lupingu Wilayani Ludewa.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

204. MHESHIMIWA AZIZA SLEYUM ALLY (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Katika nchi yetu wapo wanajeshi ambao wanaishi kwenye nyumba za jeshi na nyumba hizo hazina ubora wowote:-

Je, Serikali inajiandaaje kuwasaidia Wanajeshi wa Tabora kupata nyumba bora.

WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

205. MHESHIMIWA BAKAR SHAMIS FAKI (OLE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Tanzania itanufaika kiasi gani kwa kuridhia Itifaki ya soko la Pamoja la Afrika Mashariki.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

206. MHESHIMIWA HERBERT JAMES

MNTANGI (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji wa Misozwe umekuwa ukikwama kwa kucheleweshewa fedha za ujenzi zinazopitia Halmashauri ya Wilaya, kuharibika kwa mitambo ya ujenzi pamoja na kuondoka mara kwa mara kwa Watendaji katika eneo la ujenzi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha kasoro hizo ili mradi ukamilike haraka.

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

207. MHESHIMIWA MHONGA SAID RUHWANYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Kutokana kudorora kwa kiuchumi Serikalini ilitenga kiasi cha shilingi trilioni 3.6 ili kunusuru Kampuni Binafsi na Vyama vya Ushirika vilivyoshindwa kujiendesha kibiashara kutokana na huko kudorora kwa uchumi:-

(a) Je, ni Kampuni na Vyama vya Ushirika vingapi kwa majina na idadi yamepata kiasi gani katika Mfuko huo wa *Stimulus Package*;

(b) Je, ni kiasi gani kimetumika na kiasi gain kimebakia katika mfuko huo.

208. MHESHIMIWA MOSSY SULEIMAN MUSSA (MFENESINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Tanzania ina mpango wa Sera ya **MKUKUTA;** na kwa kuwa Tanzania inayo Mikoa ishirini na sita (26):-

(a) Je, ni Mkoa gani unaoongoza kwa umasikini nchini;

(b) Je, ni Wilaya gani inayofaa ipewe changamoto zaidi kwa sababu ya umasikini wake.

WIZARA YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:

209. MHESHIMIWA LUCAS LUMAMBO SELELII (NZEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu:- Shirika la Ndege **(ATCL)** linakabiliwa na madeni na uhaba wa Ndege kuweza kukidhi mahitaji ya usafiri ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, kuna mpango mkakati gani wa kulifanya Shirika liwe na ufanisi wa manufaa;

(b) Je, ni fedha kiasi gani kimetengwa kuwezesha **ATCL** ishindane Kimataifa.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

210. MHESHIMIWA DK. GUIDO GOROGOLIO SIGONDA (SONGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Iko dhamira ya Serikali kusambaza umeme kwenye vijiji vyote hapo nchini chini ya mpango wa “Rural

Electrification Progamme” ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake hiyo ya kutandaza nyaya za umeme kwenye nguzo zilizokwisha chimbiwa na wananchi kati ya Mji Mdogo wa Mkwajuni na kijiji cha Galula kilichoko umbali wa km. 20 tu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
12 JULAI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**